



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA JIMBO
LA KONDE NA KATA SITA

Dodoma, 3 Juni, 2021

Kiti cha Mbunge wa Jimbo la Konde, Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba kiko wazi kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Mhe. Khatib Said Haji na hivyo kukoma kuwa Mbunge kwa mujibu wa Ibara ya 71(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinamtaka Spika amtaarifu Mwenyekiti wa Tume juu ya kuwepo kwa nafasi wazi ya kiti cha Mbunge. Tayari Tume imekwishapokea taarifa hiyo kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Tume imepokea barua kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akiitaarifu juu ya kuwepo kwa nafasi wazi za Madiwani kwenye kata sita (06) za Tanzania Bara.

Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 13 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume imeandaa chaguzi ndogo ili kujaza

nafasi ya Mbunge iliyo wazi katika Jimbo la Konde na nafasi za udiwani kwenye Kata sita (06) za Tanzania Bara. Kata hizo ni:

Na.	MKOA	HALMASHAURI	JIMBO	KATA
1.	Dar es Salaam	Manispaa ya Temeke	Mbagala	Mbagala Kuu
2.	Manyara	Wilaya ya Kiteto	Kiteto	Ndirigish
3.	Mtwara	Wilaya ya Masasi	Lulindi	Mitesa
4.	Tanga	Wilaya ya Lushoto	Lushoto	Gare
5.	Mtwara	Wilaya ya Newala	Newala Vijijini	Mchemo
6.	Shinyanga	Wilaya ya Ushetu	Ushetu	Chona

Ratiba ya Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Konde na kata sita (06) za Tanzania Bara ni kama ifuatavyo:-

Na.	TUKIO	TAREHE
1.	Wagombea kuchukua fomu za uteuzi	21 - 27 Juni, 2021
2.	Uteuzi wa wagombea	27 Juni, 2021
3.	Kampeni za Uchaguzi	28 Juni - 17 Julai, 2021
4.	Siku ya kupiga kura	18 Julai, 2021

Tayari vyama vimeshapokea taarifa hii kwa barua.



Dkt. Wilson Mahera Charles

Mkurugenzi wa Uchaguzi

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI